# WALIO VUNJA UKIMYA





**kazi ya ushirikiano ya:**

*Asociación Más Mujeres* na *Save a Girl Save a Generation*

**Maandishi:** Anna Maria Porté Estop

**Michoro:** Sara Fratini

**Muundo:** María Ramis

**Toleo la Kiingereza:** Natalia Fernández Díaz-Cabal

# WALIO VUNJA UKIMYA

Hadithi hii inatokana na matukio halisi. Ukeketaji ni mila ambayo maelfu ya wanawake na wasichana kote duniani bado wanavumilia hadi leo. Hata hivyo, idadi kubwa ya wanawake wanaendelea kujinasua katika desturi hii.





Asha alimuuliza dada yake mkubwa, Zuli: “Je, iliuma?” “Yangu bado inaniwasha sana.” Zuli aliinamisha kichwa chake, akageuka na kuondoka huku akiburuta miguu yake.
Mambo yalikuwa yamebadilika tangu Asha aliporejea kutoka safari aliyoingia na mama yake kwenda kijiji cha nyanya yake. Asubuhi hiyo alikuwa na furaha; walimwambia siku hiyo itakuwa siku ya sherehe, kwamba alikuwa amekua, na wakamtuma anunue wembe. Kisha, ikatendeka.
Iliuma sana. Sasa ilikuwa inamuwasha. Ni bora asifikirie kuhusu hiyo.

Alipofunga macho, alijiona amelala chini. Ilikuwa baridi, kokoto ndogo za mchanga mkavu zikijikita mgongoni mwake, nguo iliyofunika dirisha la nyumba ikitupa vivuli kwenye kuta za udongo, vidole vyake vilipoteza hisia kutokana na vifungo, nzi wakizunguka nyumba, alihisi jasho likitiririka shingoni mwake, kisha akasikia sauti ya wembe ukikata, akaona sindano na uzi, akalia, akatamani kukimbia, lakini hakuweza.

Asha hakuelewa hiyo ilikuwa sherehe ya aina gani. Hajapenda. Hata kidogo. Ingawa nyanya yake alimwambia: *Sasa wewe ni msichana mkubwa.* Siku zimepita, na bado ilikuwa ikimuuma akitembea, akisonga, na akikojoa. Ilikuwa inamwasha. Aliuliza mama yake, walipokuwa wakienda kuchota maji kisimani, angefanya nini, na mama yake akamjibu: Osha na maji moto na chumvi. Asha alijiosha na maji moto sana karibu yaiteketeze mkono wake, lakini hakuhisi chochote. Kuwasha hakukuisha— kinyume chake, ilichomeka hata zaidi.

Asha alifikiria kuwa akiwa mkubwa, ndoo haitakuwa nzito akichota maji. Lakini akiwa miaka mitano— kweli, anadhani ana miaka mitano, akijilinganisha na urefu wa wasichana wengine wanaoenda shule— lakini hakujua kwa hakika alizaliwa lini. Hata hivyo, aliendelea kusimama mara kadhaa kwa sababu alikuwa akichoka, na siku moja aliteleza kwa sababu bado ilikuwa ikimuuma akitembea, na alimwaga maji. Labda nyanya yake alikosea. Labda bado yeye ni msichana mdogo.



Hiyo ilifanyika kwa Asha, na kabla yake, kwa nyanya yake, mama yake, na dada yake. Kwa wanawake wote wa familia. Labda hata kwa majirani. Lakini Asha hakulijua, kwa sababu hakuna aliyewahi kuzungumza kuhusu hilo. Alijaribu mara kadhaa kuzungumza na Zuli kuhusu jambo hilo. Siku moja, Zuli alipokuwa aki kata kata vitunguu ili a tayarishe pilau, alimuuliza tena: Je, ilikusumbua? Je, ita isha? Zuli alielekeza kwa sakafu, akampa yeye kitunguu, na akamwambia: *kata vipande vidogo vidogo.* Muda mfupi baadaye, Asha alimsikia dada yake akipenga kamasi, akaona mikono yake yenye vidole virefu na nyembamba ikishika leso yenye rangi nyingi, akamtazama usoni, na akagundua kwamba macho yake yalikuwa yana machozi *Vitunguu hunifanya nilie kila mara*, Zuli akasema kwa sauti ya chini. Macho ya Asha nayo yalianza kuwa na machoji. Wao wawili waliendelea kukata vitunguu huku wakilia. Na dada yake hakuwahi kumjibu.



Familia ya Asha inatoka katika jamii ya Wasomali wa Kenya. Katika maisha yake mafupi, Asha aliishi katika miji tofauti tofauti. Wazazi wake walipotengana, familia pia ilitengana: Mama yake alilazimika kutafuta kazi ili aweze kupata mahali pa kuishi. Alasiri moja, kaka yake mkubwa aliondoka kuishi na mjomba. Siku nyingine, upepo mkali ukivuma, shangazi alimchukua dada yake. Haikupita muda, mama yake akamuachia shangazi mwingine na akamwambia: *"mtoto wangu, una mashavu yanayopendeza— yameumbwa kubuswa, si kupigwa kofi. Usisahau hilo kamwe."*

Asha aliikosa sana familia yake, kiasi kwamba wakati mwingine alikuwa na matatizo ya kulala. Aliwaza kama atamwona mama yake tena, kama kaka yake bado anamkumbuka, na kama Zuli anahifadhi hadithi za kumwelezea watakapokutana tena. Hakuelewa kwa nini wote walipaswa kuishi mbali sana. Hakupenda sana kuwa katika ile nyumba — lakini kama mvua ingenyesha zaidi na vumbi lingepungua, labda haingekuwa mbaya sana. Alikuwa mdogo kuliko wote, na kila mtu alikuwa akimtuma afanye hiki na kile. Alitamani sana kwenda shule.



Muda ulipita na familia waliungana. Asha alipenda mti wa embe uliomea karibu na nyumba. Baada ya miaka mingi wakiwa mbali, mama yake alihisi kama mgeni kwake. Asha na Zuli hawakukaa naye muda mwingi. Wakati wa kula, walikuwa wakienda kwa shangazi yao, wakichota wali moto kwenye sufuria, na mikono yao ikiwa bado ikichomeka, wakikimbia kula chini ya ule mti wa embe wa zamani huku wakichekacheka. ulikuwa mti mkubwa na wa upweke — nao waliupenda sana.



Asha alihisi huzuni na hasira kidogo, kwa sababu kaka yake alikuwa akisimamia hesabu na mambo ya nyumbani kwa miaka kadhaa. Dada yake alikuwa amesoma, na mara nyingi aliandika maneno sakafuni sebuleni.

Asha alikuwa amechoka kusubiri; alihisi kwamba muda wake ulikuwa umefika. Hakuweza kwenda shule alipokuwa akiishi kwa shangazi yake, jambo ambalo lilimfanya ajisikie na hasira kwa mama yake. Hakuwa tena mtoto mdogo.

Alitamani kuelewa kwa nini mwili wake ulianza kubadilika, na aliamini kwamba labda angepata majibu ya maswali yake shuleni. Hapa nyumbani, ukimya ulimzunguka.



Mama yake Asha alishawishiwa kuolewa tena, kwa sababu waliamini kwamba mwanamke hangeweza kulea familia peke yake, hasa akiwa na watoto watatu, wawili kati yao wakiwa wa kike. Baadaye, Asha alipata dada mdogo.
Asha alimpenda sana dada yake mdogo; alimtunza na kucheza naye mara kwa mara. Hali ilizidi kuwa ngumu baada ya baba wa dada yake mdogo kuondoka, na wakabaki kuishi na mama yao pekee. Ilibidi wahame tena. Baadaye walihamia na kuishi karibu na baba yake Asha, ambaye alikuwa akija kuwatembelea na kula nyumbani pamoja na jamaa wengine aliokuwa amewaalika.
Asha alichoka kuwa wa mwisho kila mara: kutoweza kusoma, kusubiri, na kuhudumia chakula ambacho wanaume wa familia na marafiki walikuwa wakila katika chumba kikuu. Mama yake na dada yake pamoja na yeye walikuwa wakingojea mabaki kila siku.
Hadi siku moja, aliketi kwenye mkeka na kusema kwa ujasiri: "Sitaki kula mabaki tena."







Asha hakuzaliwa kuambiwa asichoweza kufanya. Kila alipoambiwa "hapana" au "huwezi kufanya", kuhusu jambo ambalo lilikuwa haki yake, alisimamia haki hiyo na alihakikisha anaithibitisha.

Siku hiyo, alivunja sheria na kuketi kwenye mkeka uliokaliwa na wanaume. Mama yake alikasirika sana, kwa sababu aliona aibu kutokana na kile alichokiona kama ukosefu wa adabu wa binti yake.

Lakini Asha hakujali aibu; alikuwa na njaa. Hakutaka kula makombo tena, na hakuelewa kwa nini wanaume walipewa chakula kwanza, ilhali yeye, dada yake na mama yao ndio waliokuwa wamekipika. Hakuna mtu aliyesema neno. Wote walimtazama kimya kimya. Kwa Asha, ilikuwa siku mpya. Mama yake alishindwa kumzuia, kwani kwa mara ya kwanza alimwona binti yake akiwa na ujasiri na msimamo. Tangu siku hiyo, mama yao aliwalisha kwanza Asha, dada yake na yeye mwenyewe, kabla ya wanaume na wageni.



Wakati huo nchini Kenya, mtoto angeweza kuanza shule mara tu alipoweza kugusa sikio la kushoto kwa mkono wa kulia au kinyume chake akipisha mkono juu ya kichwa. Kwa miaka, Asha angeweza kufikia sikio lake kwa urahisi, lakini baada ya kusihi kwa bidii aliweza kwenda shule, alikuwa mkubwa kuliko wanafunzi wote darasani— na ndiye aliyekuwa anajua kidogo zaidi. Mwishoni mwa muhula wake wa kwanza, akawa wa mwisho darasani. Wanafunzi wengine walimdharau, na kumfanya kuwa shabaha ya mizaha isiyokoma. Alirudi nyumbani huku akilia. Dada yake mkubwa, aliyeguswa na maumivu yake, alimpa kitabu kilichoitwa *"Through the Garden Gate"* na kumwambia: *"Ukitaka kujifunza kusoma, soma kitabu hiki. Ukishajifunza, hakuna mtu atakayekucheka tena."*



Tangu siku hiyo, Asha hakuwahi tena kuwa wa mwisho darasani. Alijifundisha kusoma na muda mfupi baadaye akagundua maktaba—mahali palipojaa mwanga na hadithi. Alikaa huko hadi saa za kufunga, akisoma kila kitabu alichoweza kukipata. Alikuwa na kiu ya maneno. Lakini shauku yake haikueleweka nyumbani. Kwa kuwa kulikuwa na kazi nyingi na matarajio ya kutimiza, mapenzi yake ya kusoma yalionekana kama kikwazo. "Adabu zaidi, na vitabu vichache!" familia yake ilidai.

Kila jioni alipotoka maktabani, aliadhibiwa. Hata hivyo, hakukata tamaa, aliendelea kurudi. Kadiri alivyojifunza zaidi, ndivyo alivyozidi kuamini kwamba kila msichana anastahili fursa kama hiyo. Hakuwa tayari kukata tamaa. Siku moja, mwalimu alitembelea familia yake na kusema: *"Msichana huyu ana nia nguvu na ni mwerevu. Muache asome—ana thamani sana.*



Adhabu zilikoma. Familia yake ilianza kuona uwezekano na ikaanza kufikiria jinsi ya kumuunga mkono katika masomo yake ya sekondari. Kutoka kuwa wa mwisho darasani, Asha alipanda na kuwa miongoni mwa wanafunzi bora katika mkoa mzima. Alipata ufadhili wa masomo katika shule ya bweni—ndoto ikatimia. Sanduku lake la kwanza la nguo. Taulo lake mwenyewe, mswaki, kabati na kitanda chake. Kwa siku kadhaa, shavuli kwenye shavu lake la kushoto halikutoweka kwa sababu ya tabasamu la kila wakati. Katika shule hiyo ya bweni, akiwa amezungukwa na wasichana ambao daima walikuwa na kila kitu, Asha alikuja na tamaa moja kuu: kusoma.



Ameweza kufaulu kushawishi kila mtu kwamba alikuwa mpwa wa jenerali maarufu wa Kisomali— kama msichana mwingine tu kati ya wengi. Lakini siku moja, akiwa kwenye bafu la shule ya bweni, ukweli tupu ulimgonga. Wasichana wengine walikuwa tofauti. Sio tu kwa sababu walienda kwenye kanisa la Kiprotestanti kila siku au kwa sababu walikuwa na viatu na vitabu vingi zaidi, bali kwa sababu wao hawakupitia kile alichopitia.

Ndani chumbani kwake, alianguka kitandani, akiwa amezidiwa na hisia. Inakasirisha sana! Kisha wazo likamgusa: Subiri kidogo—kumbe jambo hili halifanywi kwa wasichana wote? Kwa nini limefanyiwa mimi? Hakukuwa na mtu ambaye angeweza kuuliza.

Alianza kufanya utafiti, akitafuta katika kila kitabu alichoweza kupata, akitamani kuona maelezo. Lakini vitabu havipeana majibu. Mpasuko mkubwa ulipasua roho yake: Kwa nini walinifanyia jambo hilo? Huo ulikuwa mwili wake, faragha yake, maisha yake. Hakuna mtu aliyekuwa na haki ya kumsababishia maumivu makubwa kama hiyo.

Haijalishi kwamba ilikuwa imefanywa kila wakati, Au kwamba wazee walisema " ni nzuri kwa wasichana." Haikukuwa sawa. Walimbadilisha milele. Na sasa alijua haikuwa lazima iwe hivyo. Ungeweza kua, mwili wako unaweza badilika kwa kawaida —na hakuna mtu aliyekuwa na haki ya kuamua jinsi mwili wa mwanamke unapaswa kuwa. Abadan. Hakuna mtu. Popote duniani.

Likizo ya shule ilipofika, Asha alirudi kijijini kwa siku chache. Ili apate pesa kwa ajili ya mahitaji yake ya msingi katika shule ya bweni, alianza kuuza sambusa—maandazi yaliyojaa nyama iliyosagwa, mboga, na viungo. Asubuhi moja, alisikia kwamba mama yake alikuwa anampeleka dadake mdogo hospitalini. Walikuwa wanataka kumfanyia jambo hilo. Hapana! Asha alipiga kelele. Alijaribu kuwazuia—Si dadangu mdogo! Kamwe tena! Walimfungia ndani ya chumba. Alibisha mlango kwa masaa mengi, akipiga kelele hadi sauti yake ikapotea. Alipofunguliwa hatimaye, mama yake akamwambia kwa upole: “Sasa haiumi sana. Wanafanyia hospitalini.” Asha alimkumbatia dada yake. Hakuweza kumtazama machoni. Alimshika kwa nguvu huku dada yake akilia. Mama yake alimaanisha nini? Kwamba ikifanywa hospitalini, itakuwa bora zaidi? Hiyo ilipaswa kuifanya iwe sawa? Ni wengine wangapi walikuwa wamepitia jambo lile lile—zaidi ya dada yake, zaidi ya kijiji chake? Lakini kwa nini? Maumivu hayo yote. Ukosefu huo wa sehemu ya mwili yako. Koo la Asha liliungua—si kutokana kupiga kelele tu, bali kwa sababu ya moto uliokuwa ndani yake. Wakati huu, hakuzungumza. Hakuwa na sauti ya kutoa tena.








Asha alikuwa na ndoto ya kuwa mtangazaji wa redio. Alitaka kwenda chuo kikuu na kuwa mwandishi wa habari—kusimulia hadithi za maisha, kusema ukweli kupitia mawimbi ya hewa. Lakini hakukuwa na pesa nyumbani. Badala yake, familia yake ilipangia ndoa na mwanamume mzee anayeishi Mogadishu, mji mkuu wa Somalia. Walipojua kuwa alikuwa mjamzito, familia ya mume wake walianza kumjali. Sasa alikuwa amebeba kitu walichokiona kuwa mali yao.



Asha alitamani kuhepa hali hiyo. Wakati wa ujauzito wake, alianza kufanya kazi katika nyumba za baadhi ya marafiki wa familia yake. Aliamua: mtoto atakapozaliwa tu, atamwacha mwanaume huyo. Alisoma, akafanya kazi, na akahifadhi kila shilingi aliyoweza kupata.

Binti yake alipozaliwa—Hayat mdogo—kujifungua kulikuwa kugumu karibu Asha apoteze maisha. Lakini alipomwona uso ule mdogo, aliahidi kwa dhati: *Hayat atakuwa huru zaidi kuliko mimi nilivyokuwa.*



Asha alirudi Kenya kwa siku chache kuwatembelea familia yake, ingawa alilazimika kuenda bila Hayat. Bwana wake hajaruhusu Asha kumtoa mtoto nje ya nchi. Lakini Asha alikuwa na mpango— familia aliyokuwa akifanyia kazi walijitolea kumsaidia kubadilisha maisha yake. Pasipoti zilikuwa tayari. Mara tu akirudi, angemchukua binti yake, na pamoja wangesafiri kuhamia Denmark. Lakini kisha vita vikazuka. Mipaka ikafungwa. Hayat alinaswa. Asha hakuweza kutulizwa. Hakukuwa na habari zozote kuhusu binti yake. Alipoteza kazi yake, kipato chake, akiba yake—kila kitu. Alikuwa karibu sana kupata uhuru wake. Badala yake, alipoteza yote.

Alishindwa kulala. Hakuweza kula. Hakuweza kuhisi chochote. Vita vilimchukulia kila kitu. Siku moja, alipokuwa amepoteza mahitaji yote, alipata barua iliyotoka kwa baba yake na Hayat. Alikuwa amejaribu kufika mpakani akiwa na mtoto. Je, Asha angeweza kuwatafuta? Asha alilemewa na huzuni. Akiba yake bado ilikuwa imefichwa ndani ya godoro lililokuwa huko Mogadishu. Zuli, dada yake mkubwa, akamtazama machoni na kumwambia, "Twende tumtafute binti yako. Nitauza dhahabu yangu. Tutakwenda mpakani. Tutampata".





Walisafiri kwa kutumia malori ya misaada yaliyokuwa yakielekea kwenye kambi za wakimbizi zilizokuwa kwa mpakani. Safari ilikuwa ndefu, rasilimali zilikuwa chache. Wakafika kwenye lango lile la kutisha—lile lililotenganisha vita na amani—wakikabiliwa na mstari usio na mwisho wa miili iliyochoka na nafsi zilizovunjika. Je, watawezaje kumpata mtoto mdogo kiasi hicho katikati ya bahari hii ya watu? "Asha, amka," Zuli alisema huku akifuta machozi yake. "Hatujasafiri hii yote ili tukate tamaa. Tunarejea nyumbani na Hayat."
Wakagawanyika ili watafute Hayat. Kila uso ulianza kufanana na mwingine, Asha akasimama ghafla. Kwenye umati, aliona utepe mwekundu, uliolingana vyema na gauni dogo. Pale, karibu na nyota hiyo ndogo iliyong'aa, alisimama mume wake—akiwa mchafu, dhaifu, amebaki ngozi na mifupa pekee.

Na pale kulikuwa na Hayat. Hakuwahi kuona kitu cha kupendeza zaidi maishani mwake kuliko binti yake katika wakati huo, akiwa amesimama katikati ya vurugu. Miaka imepita tangu siku ile, lakini mwangaza uliotoka wakati huo bado unamshikilia Asha. Alijua wakati wa kuzaliwa Hayat—wakati hiyo mkono ndogo iliposhika kidole chake kwa nguvu: huyu ndiye sababu yangu. Na hapo, katikati ya ukiwa wa kutisha sana, akaweka kiapo kingine: Hakuna mtu yeyote atakayewatenganisha tena.

Asha hangeweza tena kumruhusu mtu yeyote aamue ataishi na nani au namna atakayoishi. hiyo sura imefungwa. Binti yake alikuwa na haki ya kukua huru—huru kutokana na mzigo wa mila, matarajio, na hofu. Huru ya kuota ndoto na kuchagua njia yake kibinafsi. Wakati mwingine, Asha aliogopa kwamba asingeweza kumshika yeye tena. Sasa kwa kuwa walikuwa wameungana tena, hangekubali kujiangusha. Angetafuta kazi, apate mafunzo, na ajielimishe—si kwa ajili yake tu bali pia kulinda mustakabali wa binti yake. Hakuna mtu yeyote ambaye atawahi kuumiza Hayat kama vile Asha alivyoumizwa. Hayat atasoma. Atafanya kazi. Ataolewa na yule ambaye yeye mwenyewe atachagua.

Asha alipumua kwa nguvu, bila kujua kwamba kumbatio lake la nguvu lilikuwa limemhofisha binti mdogo. Akailegeza mikono yake kidogo, akarekebisha utepe uliokuwa umevia kichwani mwa Hayat, kisha akamtazama usoni— akiuona si uso wa mwanawe tu, bali wa kila msichana anayenusurika kila siku katika dunia ambayo mara nyingi imepangwa kinyume chao. Ilikuwa wakati wa kutoka. Wakati wa kuondoka hapo. Alipangusa vumbi kwenye gauni la Hayat, akambeba, kisha akaanza kumtafuta dada yake. Wangesaidiana kupata tena njia ya kurudi nyumbani..



Asha alitalikiana na baba yake Hayat na akaenda kuishi Nairobi pamoja na Zuli na binti yake mdogo. Alipata kazi katika shirika lisilo la kiserikali lililokuwa likiwasaidia wakimbizi waliokimbia vita Somalia. Alipokuwa akiwasaidia wengine kupata makazi mapya, naye pia alikuwa akijijengea makazi yake kimya kimya.

Zuli mara nyingi alipika halwa, kitafunwa kitamu ambacho Hayat alipenda sana. Ilikuwa sababu nzuri kwa dada hao kukutana, kushiriki chai na kuzungumza kuhusu maisha yao. Alasiri mmoja, Asha alipokuwa akimpea Hayat halwa na biskuti, aliona jinsi binti yake alikuwa amekua. Labda, alifikiri, ulikuwa wakati wa kuvunja ukimya. Alimuangalia Zuli. Kwa kuwa sasa wote wawili walikuwa mama, huenda hatimaye wangeweza kuzungumzia jambo hilo—kuhusu yale yaliyowafanyiwa.

Asha alimfuta Hayat mdomo kwa kitambaa taratibu, kisha akakaa wima na kumtazama dada yake machoni. “Sitaruhusu Hayat apitie yale waliyotufanyia sisi. Kamwe.” Zuli alikaribia mezani, akaingiza kijiko alichokuwa nayo kwenye bakuli la xalwo, kisha akageukia upande wa dirisha. “Sina mabinti bado,” alisema kwa sauti ya chini, “lakini ningekuwa nao, nisingekubali wapitie maumivu hayo pia.” Huo ulikuwa mwanzo wa mazungumzo mengi. Walisikilizana. Walipata maneno ya kueleza jinsi walivyohisi wakati ule—na jinsi lilivyowaacha alama ya kudumu moyoni mwao.



Asha hakusimama hapo. Alianza kuzungumza na wanawake wengine wa familia, na pia majirani waliokuwa na mabinti. "Sitaki jambo hili limtokee mwanangu," aliwaambia. Kauli hiyo rahisi ikawa mbegu ya Save a Girl, Save a Generation.

Ilizaliwa kutokana na ufahamu wa Asha kwamba kile ambacho wanawake walihitaji ni nafasi— sehemu ambapo wangeweza kuzungumza, kushirikiana na kusema bila hofu: "Ukiokoa msichana mmoja, unaokoa kizazi kizima." Licha ya uzito wa mila na upinzani wa jamii, Asha aliona mwanga wa uwezekano mpya. Mambo yangeweza kuwa tofauti. Ukimya Asha aliouvunja haukuwa wake peke yake—ulikuwa sauti uliopaa ukimya wa mamia ya wanawake duniani kote waliothubutu kuishi kwa njia tofauti. Kwa sababu kuna zaidi ya njia moja ya kusonga mbele maishani.

Kwa sababu kuna zaidi ya njia moja ya kusonga mbele maishani. Na kama asemavyo Asha: "Hadithi ya maisha yangu imeandikwa kwenye miguu yangu. Sijawahi kuweza kushona hata kifungo. Kila mara nikiona sindano au uzi, narudishwa wakati huo.

Lakini nina hakika—pamoja, tunaweza suka masharti yanayohitajika kumaliza desturi hii. Je, utaungana nami?"



# ASHA ISMAIL NA SAVE A GIRL SAVE A GENERATION

Maisha ya Asha yalibadilika tena alipokuwa tena Alishi kwa muda nchini Ecuador huko Amerika Kusini na Tanzania, kabla ya kuhamia nchini Hispania. Hapo alikutana na wahudumu wa afya ambao hawakujua namna ya kuwahudumia waathirika wa ukeketaji. Ndipo akaamua kwamba wanawake waliotajwa na madhara ya ukeketaji wanahitaji msaada, na kwamba wangestahili kusikilizwa na kushirikiana nao katika safari yao ya kupona.

Alijigundua pia kwamba ukimya unaozunguka ukeketaji haukuwa tu kwa jamii yake—ulikuwa tatizo la kimataifa. Mamilioni ya wanawake duniani kote waliathirika na tendo hili, na utafahamu mdogo uliendelea kulifanya liendelee.

Utambuzi huu ndio uliokuwa msingi wa kuanzishwa kwa Save a Girl Save a Generation. Ikawa daraja kati ya Kenya na Hispania—ushirikiano wa pande mbili unaolenga kukuza uelewa, kuimarisha sheria, shule na vyuo vikuu, na kuendelea kutoa

mafunzo kuhusu jinsia, ukeketaji, na kusaidia wanawake ambao wamenusurika na uzoefu huu.



## Waathirika Wengine Waliojitolea Kupigania Dunia Isiyo na Ukeketaji



### Reene Bergstrom

Daktari kutoka Marekani na aliyenusurika ukeketaji.



### Nawal El Saadwi

Mwanaharakati wa kifeministi kutoka Misri, daktari na mwandishi; Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Afya ya Jamii nchini Misri.



### Masooma Ranalvi

Wakili kutoka India na mwanzilishi wa shirika la *We Speak Out*.





### Patricia Tobón Yagarí

Wakili kutoka jamii ya asili ya Emberá, mshiriki wa Tume ya Ufafanuzi wa Ukweli nchini Kolombia.



### Waris Dirie

Mwanamitindo wa kimataifa, mwandishi na aliyekuwa Balozi Maalum wa Umoja wa Mataifa dhidi ya ukeketaji.



### Adriana Kaplan

Mtaalamu wa anthropolojia kutoka Argentina, mwanzilishi wa Wassu Gambia Kafo.



### Sophia Abdi Noor

Mbunge wa Kenya aliyechangia kuendeleza sheria dhidi ya ukeketaji.



### Ifrah Ahmed

Mwanaharakati wa Kisomali raia wa Ireland na mwanzilishi wa Ifrah Foundation.

# KUZALIWA KWA HARAKATI

**Save a Girl Save a Generation** ni shirika lisilo la kiserikali linalopigania kukomesha ukeketaji, unyanyasaji wa watoto, ndoa za kulazimishwa, na aina zote za ukatili dhidi ya wanawake. Shirika hili lilianzishwa na kuongozwa na Asha Ismail mwaka wa 2007, inaongozwa na wanawake ambao walinyimwa haki ya kuzungumza na kujilinda walipokuwa watoto. Dhamira yao ni kuhakikisha kwamba hakuna msichana mwingine atakayevumilia kile walichopitia. Tangu kuanzishwa, shirika hili limeanza miradi mingi nchini Kenya na Hispania, ikisaidia kuzuia ukeketaji kwa wanawake na wasichana wengi. Pamoja na mashirika mengine, limeunda nyenzo za elimu na vitendo ili kuongeza ufahamu na kuhamasisha mabadiliko:

- How to Talk About Female Genital Mutilation:

https://www.saveagirlsaveageneration.org/imagenes/2022/11/How-to-talk-about-FGM.pdf

- Getting to Zero Female Genital Mutilation in Africa:

https://au.int/sites/default/files/documents/42276-doc-GettingtozeroFGM-FinalWebPages-small.pdf

- CHAIN Intervention: FGM and Forced Marriage:

https://www.saveagirlsaveageneration.org/imagenes/2022/11/CHAIN_Intervention-chain_Madrid_ENG.pdf

- Mariama – Story and Videol - Watch on YouTube:

https://unaf.org/publicaciones/cuento-mariama/mariama-ingles/

https://www.youtube.com/watch?v=yfm2HCroOtc

- UNICEF Technical Guidance on FGM and Education:

https://www.unicef.org/media/108641/file/FGM-Education-Note-English-2021.pdf




# HADITHI KUTOKA MKUSANYIKO WA VALIENTAS

Mkusanyiko wa VALIENTAS ni mfululizo wa hadithi zilizo na michoro unaoangazia wanawake wa kisasa wanaojenga dunia bora. Kila kitabu huunganisha picha na simulizi ili kuwasilisha hali ngumu ya matumaini na huruma, ikivutia watu wengi wa kujiunga na harakati za mabadiliko.

**PROTECTORAS:** Juzuu ya kwanza, inayoangazia watetezi wanawake wa haki za binadamu katika Abya Yala (Amerika ya Kusini) ambao wanalazimishwa kuhama maeneo yao wanapokabiliana na makampuni makubwa ya kimataifa ya uchimbaji wa rasilimali.

**PODEROSAS:** Juzuu ya pili, inayoonyesha kundi la maigizo Las Poderosas na wanawake wengine wa Guatemala waliotumia sanaa ya maonesho kubadilisha waathirika kuwa walionusurika kutokana na ukatili wa kijinsia.



# KWA NINI HADITHI HII NI YA MUHIMU?

Ukeketaji ni moja ya ukiukaji mkubwa zaidi wa haki za binadamu za wanawake na wasichana. Ni desturi yenye mizizi ya mfumo dume, inayozuia na kufafanua majukumu ya wanawake katika jamii.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linafafanua ukeketaji kama taratibu zinazohusisha uondoaji wa sehemu au jumla wa sehemu za siri za nje za kike, au majeraha mengine kwenye viungo vya uzazi, kwa sababu zisizo za kimatibabu. Ukeketaji una madhara makubwa kwa mwili na hisia za msichana au mwanamke. Unaweza kusababisha kutokwa damu nyingi, maambukizi, maumivu wakati wa tendo la ndoa, ugumu wa kupata furaha ya kimapenzi, matatizo wakati wa kujifungua, na wakati mwingine hata kifo.

Leo hii, zaidi ya wanawake na wasichana milioni 230 duniani kote wamekeketwa, wengi wao wakiwa katika nchi takribani 30—ambazo 22 zipo barani Afrika, Mashariki ya Kati, na baadhi ya sehemu za Asia. Hizi si takwimu pekee, bali ni maisha halisi—milioni 230 ya maumivu na uvumilivu.

Ingawa ukeketaji umepigwa marufuku katika nchi 44, bado unaendelea kwa siri. Wakati mwingine, wasichana husafirishwa kuvuka mipaka kutoka nchi ambazo zimepigwa marufuku hadi nchi ambazo bado unaruhusiwa.

Pia, kutokana na uhamiaji wa watu, ukeketaji umeenea hadi Marekani, Kanada, Ulaya, Australia, na New Zealand. Hii inaonyesha jinsi jamii mara nyingi hazina ufahamu na utayari wa kushughulikia na tatizo hili.

Mkataba wa Istanbul (Baraza la Ulaya wa Kuzuia na Kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Ukatili majumbani), unaotumika tangu tarehe 1 Agosti 2014 na tayari umethibitishwa na Hispania, ndiyo chombo cha kwanza kisheria barani Ulaya inayoshughulikia aina zote za ukatili dhidi ya wanawake—ikiwemo ukeketaji. Inadai kwamba nchi kuchukua jukumu kamili la kuzuia, kulinda, na kuchukulia hatua za kisheria.



# WALIO VUNJA UKIMYA : HADITHI YA UJASIRI

WALIO VUNJA UKIMYA ni hadithi ya mwanamke aliyeamini kuwa mambo yangeweza kubadilika— aliyethubutu kumzuia binti yake kukeketwa. Ni ushuhuda wa nguvu zake, safari yake ya kutafuta sauti yake mwenyewe, na ukarimu wake wa kushiriki mafundisho yake ili kubadilisha maisha ya wengine.

Asha Ismail anasimulia uzoefu wake wa ukeketaji si kwa ajili ya kukumbuka maumivu yake tu, bali kwa lengo la kamaliza matendo haya kabisa. Safari yake inaendelea kuwatia moyo wanawake wengine tangu siku alipomlinda bintiye Hayat kutokana na hali hiyo hiyo. Hadithi yake, kwa kweli, ni hadithi ya mamilioni ya wanawake.

Duniani kote, wanawake jasiri na wabunifu wamefanya ukiukaji huu wa haki za binadamu uonekane wazi na wameanzisha mabadiliko ya kuupinga. Tarehe 6 Februari inatambuliwa kuwa Siku ya Kimataifa ya Kutovumilia





Ukeketaji. Lakini vita hivi bado havijaisha.. Hadithi hii inatuita—kupitia huruma, ufahamu, na mshikamano wa udada—kutembea pamoja na Asha na wanawake wengine wengi kukomesha aina zote za ukeketaji kabisa.

Saidia Dhamira Hii. Kupitia mapato yatakayopatikana kutokana na mauzo ya Groundbreaking Girls, tutatoa msaada wa kifedha kwa shirika la Save a Girl Save a Generation, ili liendelee na kazi yake ya elimu na uzuiaji katika dhamira ya kukomesha ukeketaji. Kwa sababu tunataka shirika hili liendelee kulinda vizazi vijavyo.

Asociación MÁS MUJERES
www.masmujeres.org

**Facebook:**
Colección Valientas–Más Mujeres

**Instagram:**
@masmujeressarea





## CHOMBO CHA MABADILIKO

Hadithi hii iliyo na michoro WALIO VUNJA UKIMYA inatuonyesha—kupitia simulizi la kweli—kwamba mabadiliko yanawezekana, na kwamba dhuluma inaweza kuzuiliwa. Inatupa msukumo kuinuka na kupaza sauti: Si msichana mwingine hata mmoja zaidi!

Inatuhimiza tulinde utu wa mwili na hisia za kila msichana na mwanamke ulimwenguni.

Kama zilivyo hadithi zote katika Mkusanyiko wa VALIENTAS, hii ni zaidi ya simulizi tu—ni chombo cha kubadilisha fikra na kugusa mioyo, na cha kuvutia watu wengi zaidi kushiriki ujengo wa dunia ambayo wanawake wanaishi bila aina yoyote ya ukatili.

